PROGRAMU YA KUIMARISHA UONGOZI WA UTUMISHI WA UMMA KATIKA UTANDAWAZI

(*Enhancing Public Service Leadership in the Globalization Era Programme - EPSL*)

Utangulizi

Wazo la kuanzisha mfuko wa ufadhili wa mafunzo kwa Watendaji Wakuu na kuanza kutekelezwa kwake mwaka 2002, lilitokana na kikao cha pamoja kati ya Mhe. Rais Mstaafu William Benjamin Mkapa na umoja wa Watendaji Wakuu wa sekta binafsi. Makubaliano yalifikiwa ya kuiwezesha zaidi serikali kushirikiana na sekta binafsi nchini ili kuendeleza uchumi katika soko huria.

Tarehe 8 Oktoba, 2007, Mhe. Jakaya M. Kiwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikutana na umoja wa sekta binafsi nchini na kuzindua rasmi Bodi ya wadhamini ya Mfuko wa Mafunzo kwa Watendaji Wakuu na Kuimarisha Uongozi wa Utumishi wa Umma katika Utandawazi.

Uratibu na Usimamizi wa programu ya EPSL

Mfuko wa ufadhili wa mafunzo wa Watendaji Wakuu ulianzishwa ili kusimamia Mpango wa Kuimarisha Uongozi wa Utumishi wa Umma katika Utandawazi na mipango mingine itakayopangwa kutekelezwa.

Usimamizi wa shughuli za Mfuko wa Ufadhili wa Mafunzo wa Watendaji Wakuu ni wa pamoja kati ya watendaji wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanznaia, na Sekta Binafsi.

Programu ya Kuimarisha Uongozi wa Utumishi wa Umma katika Utandawazi unachangia na kuendeleza majukumu makubwa yanayotekelezwa na serikali na nchi hisani katika kuendeleza uchumi wa nchi.

Utekelezaji wa programu ya Kuimarisha Uongozi wa Utumishi wa Umma katika Utandawazi utagharimu dola za kimarekani milioni 2.3 na utatekelezwa kwa muda wa miaka 3 kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania, Jumuiya ya Watendaji Wakuu wa Sekta binafsi (CEOrt) na Benki ya Dunia .

Uhalali na Madhumuni ya Programu :

Madhumuni ya kuanzishwa mafunzo haya ni kuwa na utaratibu wenye ubunifu katika kutoa mafunzo kwa watendaji wakuu kutoka katika sekta binafsi na sekta ya Umma ili waweze kukabiliana na changamoto na mabadiliko yanayojitokeza katika mazingira ya biashara yanayobadilika . Mafunzo haya yana lengo pia, kuongeza uelewa wa watedaji wakuu wa sekta binafsi na sekta ya Umma kuhusu majukumu ya sekta ya Umma na ya binafsi katika uchumi na huduma za kijamii na kuboresha maisha ya jamii ya watanzania.

Madhumuni mahususi :

- Kutela mabadiliko katika utaratibu wa utendaji kazi serikalini na hasa ya ushirikiano kati ya serikali na sekta bisafsi ndani na nje ya nchi
- Kujenga uwezo wa watendaji wakuu katika sekta ya Umma na kuhimiza utendaji unaojali matokeo.

Washiriki.

Washiriki katika programu hii ni watendaji wakuu katika sekta ya umma wanaohusika na mabadilliko ya sera katika ngazi za uongozi serikalini na watendaji wakuu katika sekta binafsi.Hawa ni pamoja na :

- Makatibu Wakuu
- Washauri wa Sera
- Makamishna na wakurugenzi
- Wakuu wa idara za serikali na wakala
- Watendaji wakuu na maofisa wakuu katika sekta binafsi.

Utaratibu unaotumika katika utekelezaji wa programu.

Programu ya kuimarisha uongozi wa utumishi wa umma katika utandawazi inatekelezwa kwa njia mbalimbali.

Hatua ya kwanza inakuwa ni ya majadiliano ya vikundi ambapo maafisa waandamizi hujadili mambo muhimu yanayohusiana na mahusiano, wajibu na majukumu yao.

Hatua ya pili inahusu kuwa na watoa mada wenye uzoefu unaotakiwa kualikwa kutoka nchi nyingine kuja kutoa mada kuhusu ushirikiano kati ya sekta binafsi na serkali.

Hatua ya tatu ni vikundi kutathmini na kufanya ulinganisho wa hali ilivyo kiutendaji ikilinganishwa na utendaji katika nchi nyingine.

Mambo ambayo washiriki wamefaidika nayo kutokana na mafunzo haya:

Hadi sasa, jumla ya maafisa waandamizi 70 kutoka katika sekta ya umma na binafsi wamefaidika na programu hii ambayo imefanyika kupitia vipindi vya majadiliano ya vikundi ambapo makundi manne tofauti yalihudhuria kwa muda wa siku tano kwa kila kundi.

Njia mbalimbali zenye ubunifu wa kuweka bayana mambo mbalimbali muhimu bila kutumia vitabu vya rejea zilitumika kujadili na kufafanua mambo yafuatayo: Mamlaka na utaalam, ushindani na ushirikishwaji, kuainisha na kutafuta ufumbuzi na ushiriki.

Mafunzo muhimu yaliyoweza kupatikana ni kama ifuatavyo:

1. Uamuzi anaoutoa kiongozi ni muhimu. Ni muhimu kuwajengea viongozi uwezo wa kufanya maamuzi.
2. kukubali tofauti zilizopo kunawezesha viongozi na jamii kuwa na maelewano na hali ya amani.
3. kusikiliza na kupokea maoni ya wengine ni jambo muhimu katika uongozi.
4. Daima tunaweza kuleta mabadiliko ya hali tuliyonayo.
5. Watu huiga na kufuata wanayoyafanya viongozi. Viongozi ni vema wakajali jinsi na mambo wanayoyafanya.
6. Mambo mengi ambayo viongozi wanayachukulia ya kawaida yamechukua muda na jitihada za wengine waliotangulia.Viongozi wajitahidi kufanya kazi zaidi ili kuwepo kwao kutokane na kukubalika na jamii.
7. Kufikia malengo na matarajio ya maendeleo kunatokana na juhudi za kila mtu mmoja. Kufikiwa kwa malengo ya kila mmoja ndiyo kufikiwa kwa mafanikio ya jamii nzima.
8. Mazingira huru ya kuchangia mawazo na maoni huwezesha watu kuwa na ushiriki mzuri. Hali hiyo huwafanya watu kuona wanathaminiwa na kuongeza ushiriki wao.
9. Uongozi mzuri ni ule unaozingatia mazingira ya mahali husika. Mbinu na staili ya uongozi iendane na hali ya mahali husika.
10. Ilikuwa wazi kwa washiriki wote kwamba matokeo mazuri na maisha bora kwa watanzania yatatokana na :-
    a. Kuengezeka kwa ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.
    b. Sekta binafsi kuwa yenye ari na ujasiri na kutumia fursa mbalimbali kwa manufaa ya nchi.

c. Kuwa na jamii isiyokubali misingi ya rushwa ni muhimu kwa mafanikio ya sekta binafsi ili kuongeza mchango wa sekta binafsi katika ukuaji wa uchumi.

d. Jamii isiyo na rushwa ni muhimu kwa ufanisi wa sekta ya umma na kukua kwa sekta binafsi katika kuchangia uchumi wa nchi.

e. Majadiliano ya kila mara kati ya sekta binafsi na sekta ya umma .

11. Ilikubalika kuwa ni muhimu kwa serikali kupitia mafanikio ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, na inapobidi kufanya marekebisho ya mikakati na mipango iliyopo.

Kwa kuzingatia tathmini isiyo rasmi na maoni ya washiriki baada ya ushiriki, programu hii imeonyesha mafanikio. Mabadiliko tarajiwa katika sekta ya umma yataonekana katika mabadiliko ya kimtazamo na kiutendaji. Mabadiliko haya yanaweza yasiwe ya kuonekana mara moja, hata hivyo, mafanikio haya ni mwanza mzuri wa matarajio makubwa ya mabadiliko tunayoyatazamia siku zijazo.